**BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR**

Simu Nam. + 255 24 2230602/1
Fax Nam. + 255 24 2230215
Tovuti: www.zanzibarassembly.go.tz

SANDUKU LA BARUA 902,
ZANZIBAR
Barua Pepe: zahore@zanlink.com

# HOTUBA YA MAONI YA KAMATI YA FEDHA, BIASHARA NA KILIMO KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO KWA MWAKA WA FEDHA 2016/2017.

**Mheshimiwa Spika,** napenda kuchukua nafasi hii kutanguliza shukrani zangu za dhati kwa Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama mbele ya Baraza lako tukufu katika hali ya uzima na afya njema katika mkutano huu wa pili wa Baraza la tisa. Aidha, napenda kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii adimu na adhimu kuweza kuwasilisha maoni ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya Bajeti ya Wizara ya Fedha kwa mwaka wa fedha **2016/2017**.

**Mheshimiwa Spika**, Nichukukuwe nafasi hii pia kumshukuru na kumpongeza Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Dkt, Khalid Salum Mohamed, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu pamoja na watendaji wengine wote wa Wizara hii kwa mashirikiano yao ya dhati kwa Kamati wakati tulipokua tukiipitia makadirio na mapato ya Wizara hii.

**Mheshimiwa Spika,** niruhusu pia nitoe shukrani za aina ya pekee kwa wananchi wote wa Jimbo la Fuoni kwa kunichagua kwa kauli moja kuwawakilisha katika Baraza lako tukufu la kutunga sheria.Namuomba mwenyezimungu anifanyie wepesi katika kuitumikia dhamana hii ya uwakilishi.

**Mheshimiwa Spika**,sitakuwa nimetenda haki iwapo nitaendelea na hotuba hii bila ya kutoa shukrani za pekee kwa waheshimiwa wajumbe na makatibu wa kamati yangu, ambao tumeshirikiana kwa umoja wetu kuyapitia na kuyachambua makadirio haya ya Bajeti ya Wizara hii na hatimae kuyakubali pamoja na marekebisho tuliyoyafanya.

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuheshimu, kuthamini na kutambua mchango wao wakati kamati ilipokua ikifanya kazi iliyokusudiwa, naomba niwataje kwa majina kama ifuatavyo:-

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Mhe. Yussuf Hassan Iddi | - | Mwenyekiti |
| 2. | Mhe. Hamida Abdalla Issa | - | Makamo Mwenyekiti |
| 3. | Mhe. Ussi Yahya Haji | - | Mjumbe |
| 4. | Mhe. Ali Salum Haji | - | Mjumbe |
| 5. | Mhe. Hamad Abdalla Rashid | - | Mjumbe |
| 6. | Mhe. Moh'd Mgaza Jecha | - | Mjumbe |
| 7. | Mhe. Bihindi Hamad Khamis | - | Mjumbe |
| 8. | Mhe.Shadia Mohamed Suleiman | - | Mjumbe |
| 8. | Ndg. Salum Khamis Rashid | - | Katibu |
| 9. | Ndg. Abubakar Mahmoud Iddi | - | Katibu |

**Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha **2015/2016**, Baraza la Wawakilishi liliidhinishia Wizara ya Fedha matumizi yenye jumla ya **172,076.6** milion. Fedha hizo zilijumuisha matumizi ya **TZS 72,199.00** milioni ya **FO1, TZS 83,548.70** milioni ya FO2 pamoja na **TZS 16,328.90** milioni ya FO3. Vilevile , kwa mwaka wa fedha **2015/2016** Wizara iliidhinishiwa kukusanya jumla ya **TZS 817,269.14** milion ambao hadi kufikia Machi, **2016** Wizara ilikua imeshakusanya jumla ya **381,483.36** milioni ambazo ni sawa na asilimia **47** ya makadirio ya mapato kwa mwaka.

**Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa ukusanyaji wa mapato kwa mwaka 2015/2016, kamati yangu haikuridhishwa kwani asilimia **47** zilizokusanywa kutoka Wizara ya fedha kupitia vyanzo vyake mbalimbali hadi kufikia mwezi Machi 2016.Mheshimiwa Spika, Wizara hii ni wizara kiongozi inatakiwa iwe ya mfano hasa kwenye makusanyo ya mapato.Hivyo Wizara ijitahidi kutumia mbinu mbadala ili kuhakikisha mwaka huu wa fedha 2016/2017 ifikie angalau asilimia **80** hadi kufikia mwezi wa machi 2017.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati yangu ina imani kubwa na Wizara hii hasa ukizingatia hii ndio Wizara mama katika kuinua hali za wananchi. kwa mwaka wa fedha **2016/2017** Wizara ya Fedha imepangiwa kukusanya jumla ya **TZS, 824,355,600,000** na kutumia jumla ya **TZS 68,249,529,000** ambalo ni fungu **F01.** Aidha inakadiriwa kutumia jumla ya **TZS 83,529,900,000** kwa ajili ya utekelezaji wa Fungu F02 ambao ni mfuko Mkuu wa Serikali na **Fungu FO3** ni jumla ya **TZS 5,911,978,000**. Aidha Wizara imejipangia kutekeleza Programu Kuu

tatu na Programu ndogo kumi pamoja na huduma na shughuli mbalimbali ambazo zitakazowezesha kufanikisha bajeti hii.

**Mheshuimiwa Spika**, Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo inaishauri Wizara ya Fedha kuwa makini na matumizi ya fedha zitakazoingizwa katika Programu hizo kwani licha ya uhaba wa fedha tulionao hivi sasa, matokeo ya fedha zitakazoingizwa yatahitaji kuonekana na kupimwa kwa umakini na ufanisi mkubwa hususan katika utekelezaji wa Programu hizo muhimu ambazo Wizara imeona ndio kipaombele chake.

**MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA (TRA)**

**Mheshimiwa Spika,** kwa kipindi cha july 2015 mpaka Juni 2016 mamlaka ya mapato ilipangiwa kukusanya jumla shilingi million **178,600.00** ambayo hadi machi ilifikia asilimia 68% ya mapato hayo**.**

**Mheshimiwa Spika,** Pamoja na utekelezaji mzuri wa malengo ya taasisi hii, Kamati inaitaka Mamlaka hii ya Mapato kuzidi kujiapanga vizuri ili kwenda na wakati wa karne hii ya sayansi na teknolojia ili kuweza kudhibiti udanganyifu unaofanywa na baadhi ya wafanyabiashara wasio waaminifu kwa mashirikiano na baadhii ya watendaji wanaoweza kutoa taarifa zisizo za kweli kuhusu aina, wingi na gharama za bidhaa zao wanapoingiza bidhaa hizo hapa nchini kwani kufanya hivyo kunaikosesha sana mapato Serikali ambayo yanahitajika katika shughuli mbali mbali za kimaendeleo hapa nchini.

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na kadhia hiyo ya udanganyifu uliokithiri, Kamati inaitaka Wizara na Mamlaka hii kutochelewa kumchukulia hatua mtendaji yeyote anaebainika kushiriki au kusababisha udanganyifu na upotevu wa mapato ya Serikali ili kudhibiti kikamilifu nidhamu ya uwajibikaji ukusanyaji wa mapato ya Serikali.

**BODI YA MAPATO (ZRB)**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati yangu imegundua kuwa, miongoni mwa maeneo ambayo mapato ya nchi yanapotea kwa wingi ni katika sekta ya utalii, hii inatokana na taarifa zinazotolewa na wamiliki wa Hotel sio sahihi. Hivyo Kamati inaishauri Wizara ya Fedha na Mipango kupitia

Bodi yake ya mapato kufanya ziara za mara kwa mara katika mahoteli ili kuhakikisha idadi halisi ya wageni wanaofika katika hoteli hizo.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati pia imeishauri Wizara kuchukua hatua kali kwa watendaji wa bodi ya mapato ambao sio waadilifu na wanaosababisha mapato ya nchi kuvuja kwa lengo la kujinufaisha na kupata utajiri wa haraka kwani imebainikiwa kuwa watendaji wa Bodi ndio wanaoshirikiana na wamiliki wa hoteli hizo katika kukwepa kulipa kodi.

**Mheshimiwa Spika,** naomba ieleweke kwamba uchumi wa visiwa hutegemea sana rasilimali za ndani hivyo Kamati inaishauri Wizara ya Fedha kupitia Bodi ya Mapato kuwa wabunifu na kuweza kuanzisha vyanzo vipya vya ukusanyaji wa mapato ili kuongeza mapato ya ndani yanchi na kupunguza utegemezi wa wafadhili.

**Mheshimiwa Spika,** suala la kutoa elimu ya kulipa kodi kwa wananchi ni jambo muhimu na la msingi sana hasa ukizingatia wananchi wengi hawajui umuhimu wa kodi anayolipa ndio maana hata wanaponunua bidhaa katika maduka au kwa wafanya biashara hua hawadai risiti zao hivyo hupelekea kukosekana kwa pato la Serikali. Hivyo, Kamati inashauri Elimu ya mlipa kodi iwe endelevu kupitia vituo mbalimbali kama redio, televisheni, mitandao ya kijamii na hata katika shehia zetu.

**Mheshimiwa Spika,** nchi yeyote duniani bila ya kukusanya kodi haiwezi kupata maendeleo yoyote, unapozungumzia maendeleo ya jamii maanayake ni kodi,tunapozungumzia maji safi maana yake ni kodi,tunapozungumzelimu bora, matibabu pamoja na kukua kwa uchumi wa nchi maana yake ni kodi. Hivyo maendeleo ya nchi yeyote hupatikana na ulipaji wa kodi kwani bila ya kodi Serikali haitoweza kutekeleza mipango na shughuli za maendeleo, Hivyo Kamati inaiomba Wizara katika jambo hili la kulipa kodi isiwe na muhali kila mmoja awajibike kwa nafasi yake kuhakikisha lengo la Serikali la kukusanya mapato linafanikiwa kwa asilimia 100.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati yangu imesikitishwa sana na biashara ya magendo ya mafuta, tatizo hili ni la mda mrefu na hadi leo halijapatiwa ufumbuzi.Aidha, tumepata taarifa kuwa mafuta yamekamatwa ya

magendo lakini hadi hivi sasa wahusika hawajakamatwa.Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuongeza juhudi zaidi katika udhibiti wa magendo ya mafuta hususan kwenye bandari bubu ambazo wafanyabiashara hawa wanazitumia.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaishauri Wizara ya Fedha na Mipango kurekebisha sheria ya mapato ili iweze kuwa na nguvu na mamlaka makubwa katika udhibiti kodi. Aidha kwa wale wanaopenda kujishughulisha na biashara hii ya mafuta tunawaomba wafuate sheria na kanuni zilizopo ili wafanye biashara hii kihalali kwa maslahi ya taifa letu.

**SHIRIKA LA BIMA LA ZANZIBAR**

**Mheshimiwa Spika,** Kama inavyofahamika kuwa Shirika la Bima la Zanzibar lina jukumu la kutoa huduma za Bima kwa ujumla. Hatahivyo, kwa kipindi hichi cha karibuni kumeibuka wimbi la bima feki hasa kwa upande wa vyombo vya barabarani, hii inatokana na baadhi ya mawakala wa bima kutokua waaminifu na huamua kuchapisha bima ambazo hazina stakbadhi kwa lengo la kujinufaisha wao.

**Mheshimiwa spika,** Kamati inaiomba Serikali kuanzisha msako maalum ili kuweza kuwabaini wahalifu hao ambao huitia serikali hasara na kusababisha kudhorota kwa uchumi.Zoezi hili liwe endelevu kwa shirika la Bima kufanya ukaguzi wa mawakala wao kila baada ya muda na hatua kali zichukuliwe kwa wale mawakala wasiokua waaminifu.

**BENKI YA WATU WA ZANZIBAR**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inachukua nafasi hii kuipongeza Benki ya Watu wa Zanzibar kwa huduma zake inazozitoa kwa jamii ambazo zimekua ni msukumu mkubwa kwa maendeleo ya wananchi wetu.

**Mheshmiwa Spika,** uamuzi wa Serikali wa kuwataka wafanyakazi wake wote kupokelea mishahara yao benki ulikua na kusudio la kudhubiti hali ya sintofahamu iliyokua ikitokea kwa kipindi kikubwa ambapo baadhi ya wafanyakazi walikua wakipokea mishahara mara mbili na wengine ambao wameshafariki mishahara yao ilikua ikipokelewa na watu wengine. Hivyo, uamuzi huo ulifanywa kwa nia njema kabisa na hatimae kudhibiti mapato ya Serikali na sio kuwasumbua wananchi

ambao wengi wao kwa hali ilivyo hivi sasa wamakua wakisumbuka wakati wa kupokea mishahara yao.

**Mheshimiwa Spika**, Kutokana na msongamano mkubwa unaokuwepo kila mwisho wa mwezi katika ATM zilizopo hivi sasa, Kamati inaona ipo haja kwa PBZ kuongeza ATM katika maeneo mbali mbali ili kupunguza msongamano na kupunguza adha ya kukosa pesa kwa baadhi ya wananchi ambao wengi wao hutegemea fedha hizo kujikimu katika mahitaji yao msingi.

**Mheshimiawa Spika,** Islamic Banking Division nayo imekua na changamoto nyingi katika utoaji wa huduma zake ikiwemo changamoto ya kuwa na foleni kubwa kila ifikapo mwisho wa mwezi, tatizo la kutofanya kazi kwa kadi za ATM kila ifikapo mwiso wa mwezi na mengi mengineyo. Kutokana na hali hiyo, Kamati yangu inachukua nafasi hii kuishauri Islamic Banking Division kufanya juhudi za makusudi za kuzifanyia kazi changamoto hizo na ikiwezekana kuziondosha kabisa ili wananchi wetu waweze kupata huduma za kibenki kikamilifu kwa wakati muafaka.

**MFUKO WA HIFADHI YA JAMII**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati yangu inunga mkono juhudi zinazochukuliwa na uongozi wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa ubunifu wao wanaoufanya wa kuanzisha miradi mbali mbali yenye lengo la kuendelea kulipa mafao kwa wanachama wake**.**

**Mheshimiwa Spika,** hii ni hatua nzuri lakini tunaishauri Taasisi hii kuwa makini katika ukusanyaji wake wa mapato katika miradi yake kama vile Uwanja wa kufurahisha watoto wa Kariakoo na Tibirinzi Pemba, mnara wa kumbukumbu uliopo Mwembe Kisonge pamoja na milango ya maduka iliyopo karibu na soko la Mwanakwerekwe na pia wawe makini katika kuisimami hiyo miradi kwa lengo la kuhakikisha inadumu na kuleta tija kama ilivyokusudiwa.

**SO1-Programu ndogo ya Mfumo wa udhibiti na Ulipaji.**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaunga mkono program hii hasa ukizingatia lengo lake ni kuhakikisha kuwa na mfumo wa udhibiti wa

mapato na ulipaji, Hatahivyo Kamati inaishauri Wizara ya Fedha kuhakikisha risiti za malipo zinafika katika maeneo husika kwa wakati na pia zinatumika kwani kumejitokeza tabia kwa baadhi ya watendaji wa Serikali hususan Pemba hufanya malipo bila ya kutoa risiti hatimae husababisha mapato ya Serikali hupotea, kwani wahenga wanasema mali bila ya daftari hupotea bila ya habari.Aidha, Serikali iharakishe ununuzi wa mashine ya EFD ili kudhibiti uvujaji wa mapato na kuongeza wigo wa ukusanyaji mapato.

**Mheshimiwa Spika,** kwakuwa Serikali ya awamu ya saba imeamua kwa dhati kubana matumizi pamoja na kudhibiti mapato ya Serikali, Kamati inaishauri Serikali kupitia Wizara ya Fedha kuwa suala la washika fedha kukaa sehemu moja (station) kwa muda mrefu ni tatizo na ndio chanzo cha kufanya kazi kwa mazoea, hivyo Wizara ijenge tabia ya kuwahamisha washika fedha kila baada ya muda kama inavyofanya kwa wahasibu ili kuepusha kujenga ngome katika sehemu moja.

**Mheshimiwa Spika**, kamati inaishauri Serikali kufanya ukaguzi mara kwa mara katika taasisi zake kwani kuna mambo mengi yanajitokeza ambayo yanaigharimu Serikali kuu kama vile wafanyakazi hewa, wastaafu hewa, safari hewa pamoja na manunuzi hewa. Mheshimiwa Spika, katika mambo ambayo nduguzetu wa Tanzania bara wameanza kufanikiwa kudhibiti mapato yao ni wafanyakazi hewa.Serikali isipokua makini jambo hili basi Wizara ya fedha haitoweza kufanikiwa malengo yake kwani itakua inajitahidi kukusanya wakati Wizara nyengine zinavujisha hayo mapato.

**SO2-USIMAMIZI WA MANUNUZI NA UHAKIKI WA MALI ZA SERIKALI**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo haina tatizo na lengo la program hii ndogo ya kuweka uwazi na usawa wa tathmini za manunuzi. Hatahivyo tunaishauri Wizara ya fedha kuhakikisha inatumia wafanyakazi ambao waadilifu katika kufanikisha zoezi hilo kwani kumejitokeza tabia kwa baadhi ya watendaji wa Serikali kuhujumu mali za Serikali kwa makusudi ili mali hizo ziuzwe kwa bei ya hasara na kunufuisha kikundi tu cha watu.Aidha, sheria ya manunuzi ina mapungufu mengi hivyo Kamati inaiomba Serikali ilete mswada wa marekebisho ya Sheria ya manunuzi ili iendane na wakati uliopo.

**Mheshimiwa Spika** , sio kila chakavu inahitaji kuuzwa, kuna chakavu nyengine zinatengenezeka tena kwa gharama ndogo tu na kwakufanya hivyo tunaweza kuokoa mali nyingi tu ambazo zilipangwa kuuzwa wakati bado ni nzima na zinaweza kutumika kwa kipindi kikubwa tu bila hata kuleta matatizo au athari kwa jamii. Aidha, Kamati inaishauri Serikali kuendelea kuhakiki mali za Serikali na kuziweka katika kitabu maalum cha kumbukumbu (Asset Register)

**SO3-TUME YA MIPANGO**

**Mheshimiwa Spika,** matumaini ya Wizara zote 13 ni Wizara ya Fedha, matumaini ya Wazanzibari ni Wizara ya Fedha, hivyo Wizara iwe na mikakati madhubuti ili kufanikisha malengo, mipango na matarajio ya Wazanzibar kwamaana hiyo Wizara ihakikishe inazisimamia kwa uangalifu program ya kupunguza umasikini, mipango ya maendeleo, usimamizi wa uchumi pamoja na nyengine kama ilivyojipangia kwa manufaa ya wananchi wa Zanzibar.

**Mheshimiwa Spika,** kamati yangu inafahamu kuwa Wizara ya fedha ina nia nzuri tu ya kuhakikisha wananchi wanakwamuka na hali ya umasikini hivyo tunaiomba Serikali kuu kuhakikisha inawapatia nyenzo na ushirikiano wa hali ya juu Wizara hii, ili kuhakikisha wanafanikiwa malengo yao waliojipangia kwani kunafanikiwa kwa Wizara hii itapelekea kufanikiwa kwa Wizara nyengine ndani ya Serikali ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

**VIPAUMBELE VYA WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO/2016-2017**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati haina pingamizi na vipaumbele vya Wizara ya fedha ila inatoa angalizo tu hasa katika kipaumbele cha miradi ya ujenzi. **Mheshimiwa Spika**, naomba ifahamike kuwa katika maeneo ambayo Taasisi zetu zinapata changamoto nyini ni wakati wa miradi ya ujenzi.Changamoto hizi hutokana na sababu mbali mbali kama vile,

1. Uwezo mdogo wa Wakandarasi,.
2. Ushirikishwaji mdogo wa wataalamu wa ndani.
3. Ubinafsi wa baadhi ya watendaji.
4. Ukiukwaji wa Sheria na Kanuni za Fedha.
5. Uwajibikaji mbovu

6. Mikataba inayotoa fursa ya kuitia nchi hasara.n.k.

**Mheshimiwa Spika,** hii imejitokeza pale kamati ilipotaka ipatiwe taarifa kuhusiana na kukwama kwa ujenzi wa jengo la tibirinzi ndipo ikapata taarifa kuwa jingo halina kiwango na mkandarasi hajulikani alipo .Hivyo Kamati inaishauri Wizara kuwa makini katika ujenzi wa miradi hii iliyojipangia ili kuepusha hasara zisizokua za lazima.Hata mradi wa Terminal II umekumbwa na changamoto na kuitia hasara Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo imeyakubali mapendekezo ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa mwaka wa fedha 2016/2017, na inawaomba Waheshimiwa Wajumbe wako wote waijadili, watoe mapendekezo yao na hatimae kuipitisha Bajeti hii muhimu.

**Mheshimiwa Spika,**
Mwisho kabisa napenda kuwashukuru Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu kwa kunisikiliza kwa makini na utulivu mkubwa wakati wote nilipokuwa nikiwasilisha hotuba hii na katika mwezi huu mtukufu wa Ramadhani. Mwenyezi Mungu aturehemu sote.

**Mheshimiwa Spika,**
Naomba kuwasilisha.

Ahsante

……………………………………
Mhe. Yussuf Hassan Iddi
Mwenyekiti,
Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo,
Baraza la Wawakilishi,